**Uteuzi wa Waombaji wenye sifa stahiki:**
Maombi yote yanayowasilishwa Wizarani na waombaji huwekwa katika kumbukumbu (database). Fomu za waombaji hupitiwa kwa umakini mkubwa na hatimaye huandaliwa taarifa ya uteuzi wa waombaji wenye sifa stahiki. Majina ya waombaji wenye sifa huwasilishwa kwenye nchi iliyotoa fursa/ ufadhili wa masomo kwa wakati. Inasisitizwa kwamba nchi husika ndiyo inatoa uamuzi wa mwisho wa nani anufaike na nafasi zilizotolewa. Kwa mantiki hiyo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ndio yenye dhamana ya kupendekeza majina ya waombaji wenye sifa na uteuzi wa mwisho hufanywa na nchi husika.

**Taarifa kwa waombaji walioridhiwa na Serikali zilizotoa Ufadhili :**
Wizara ikishapokea majina ya waombaji walioridhiwa na Serikali husika hutoa taarifa kwa wahusika na umma kupitia anuani zao, tovuti za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Vyuo Vikuu na mbao za matangazo za Wizara. Aidha, maofisa wa Idara ya Elimu ya Juu huwapigia simu waombaji walionufaika na kuwataka kufika Wizarani kupata maelezo ya hatua za kuchukua. Kwa nchi ambapo skolashipu huratibiwa na Balozi zao hapa nchini, Balozi hizo huwasiliana moja kwa moja na wanufaika ili kuwaelekeza nini cha kufanya.


**Imetolewa na:-**
Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
~~Block 10~~ Mji wa Serikali
~~Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria~~ Mtumba, Mtaa
~~Chuo Kikuu Dodoma~~ wa Afya
S.L.P 10
40479 **Dodoma,**Tanzania
Barua pepe: info@moe.go.tz
**Tovuti** (Website):http://www.moe.go.tz
Simu: +255 26 296 3533


# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



**FURSA ZA MASOMO ZINAZOTOLEWA NA NCHI WAHISANI**

## Utangulizi :

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuwa ikiratibu fursa za masomo ya Elimu ya Juu (**Shahada za Kwanza, Uzamili na Uzamivu**) zinazotolewa na nchi rafiki.

Baadhi ya nchi ambazo zimekuwa zikitupatia fursa/ufadhili wa masomo nje ya nchi ni pamoja na Uingereza, Jamhuri ya Watu wa China Jamhuri ya KoreaKusini(South Korea), Cuba Oman, New Zealand, Mauritius, Uturuki, Urusi Afrika Kusini,Algeria na Misri.

Nchi nyingine huwa zinatupatia ufadhili wa masomo kupitia kwenye Ofisi za Balozi zao hapa nchini. Mfano wa nchi hizo ni:-India, Uholanzi, Ujerumani, Sweden, Norway, Ireland, Hispania, Marekani, Ubel'giji, Finland,Ufaransa n.k. Aidha, baadhi ya nchi hutoa fursa hizo kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na zinawahusu watumishi wa Serikali tu.

Nchi hizi huwa zinawasilisha fursa hizo kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ambayo huziwasilisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya uratibu.

## Utoaji wa Taarifa kwa Umma Kuhusu za masomo na ufadhili nje ya nchi:

Taarifa za ufadhili hutolewa kwenye tovuti za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WEST)(www.moe.go.tz ), Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) (www.tcu.go.tz), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na kwenye mbao za matangazo za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## Gharama za maombi ya Skolaship :



Mwombaji wa masomo hahitajiki kulipa gharama yoyote wakati wa kuwasilisha maombi yake Wizarani au kwenye taasisi ambayo itakuwa imepewa jukumu la kushughulikia suala hilo. Hata hivyo, mwombaji aliyefanikiwa kupata fursa itampasa kulipia gharama za kupima afya, Hati ya Kusafiria na VISA ya kuingia katika nchi husika.

## Sifa za Waombaji wa Ufadhili wa Masomo nje ya nchi

Sifa za waombaji huwa zinaainishwa kwenye tangazo linalohusu Skolashipu husika. Hata hivyo sifa za jumla ni kama ifuatavyo:-

(i) Mwombaji awe Mtanzania;

(ii) Mwombaji awe na ufaulu mzuri katika masomo yake kwenye ngazi ya awali; na

(iii) Umri wa mwombaji unategemea Shahada ambayo mhusika anaomba.

## Vipaumbele vya Nchi :

Fursa na ufadhili wa masomo kutoka nchi rafiki,kuutangazia umma,huzingatia programu za vipaumbele vya taifa kama ifuatayo

- Ualimu wa Sayansi, Hisabati na Lugha ya Kiingereza;
- Sayansi za Tiba ( Health Sciences);
- Uhandisi;
- Uhandisi wa Umwagiliaji (Civil and Irrigation Engineering);
- Teknolojia ya masuala ya Mafuta na Gesi;
- Teknolojia ya habari na Mawasiliano;
- Uhifadhi wa Mazingira; na
- Mabadiliko ya Tabianchi.